**MAELEZO YA MKURUGENZI MKUU WA NEMC ALIYOYATOA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MATOKEO YA UKAGUZI WA MAZINGIRA KATIKA MIRADI YA UZALISHAJI NA MAENDELEO KATIKA KANDA YA ZIWA JIJINI MWANZA TAREHE 27/07/2016**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi (Mkuu wa Mkoa wa Mwanza),

Waheshimiwa wageni waalikwa;

- Wakuu wa Mikoa (Kagera, Geita, Shinyanga, Simiyu na Mara),
- Mkurugenzi wa Jiji Mkoa wa Mwanza
- Wakuu wa Wilaya (Kwimba, Magu, Nyamagana, Sengerema, Ukerewe),
- Maafisa Wasimamizi wa Mazingira wa Mikoa (Mwanza, Kagera, Geita, Shinyanga, Simiyu na Mara),
- Mkurugenzi Mipango Mji Mkoa wa Mwanza,
- Kamishina wa Madini Kanda Mkoa wa Mwanza,
- Wakala wa Udhibiti wa huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Mwanza,
- Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria Mkoa wa Mwanza.
- Meneja, Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria,
- Wakala wa Ukaguzi Madini Tanzania – Kanda ya Mwanza,
- Waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali nchini,
- Mabibi na Mabwana.

Napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha katika mkutano huu muhimu kama wadau wa mazingira. Aidha, napenda kuwashukuru wote kwa kuacha shughuli zenu muhimu na kufika kuhudhuria Mkutano huu.

**Ndugu Mgeni Rasmi**

Mkutano huu ambao umejumuisha viongozi wa Mikoa, Wilaya, Kanda na Wanahabari unalenga kuongeza uelewa juu ya masuala ya mazingira na uelewa

kuhusu majukumu yetu. Tumepanga kutoa taarifa fupi iliyoandaliwa kutokana na zoezi lililofanywa na Baraza la kukagua miradi ya uzalishaji na maendeleo katika Kanda ya Ziwa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mara na Kagera.

**Utangulizi: Sheria ya Mazingira na Utekelezwaji wake**

Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linayo mamlaka ya kusimamia shughuli za utunzaji wa mazingira nchini chini ya sheria No. 20 ya Utunzaji na Usimamizi wa Mazingira (EMA) ya mwaka 2004. Sheria ya Mazingira ilianza kutumika rasmi tarehe 01/07/2005.

Katika kutekeleza majukumu yake, NEMC ina mamlaka ya kukuza, kuchochea, kusimamia na kuunganisha masuala yote yanayohusiana na mazingira. Hivyo, Baraza linawajibika kuhakikisha kuwa Mazingira yanatunzwa ili kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali kwa ajili ya ustawi na maisha bora ya Wananchi wa Tanzania. Katika kufanikisha utunzaji wa Mazingira, baadhi ya mambo ambayo Baraza linahusika nayo ni pamoja na yafuatayo:

i. Ukaguzi wa mazingira na kutoa maelekezo mbalimbali yanayolenga kuboresha hali ya mazingira au kutoa makatazo mbalimbali ya kisheria yanayolenga kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa mazingira;

ii. Kufanya mapitio ya taarifa ambazo zitasaidia katika hifadhi na usimamizi wa ubora wa mazingira;

iii. Kufanya na kuratibu utafiti na uchunguzi kwenye mazingira ili kukusanya na kusambaza taarifa kuhusu matokeo ya utafiti na uchunguzi huo;

iv. Kupitia na kutoa mapendekezo juu ya kupitisha taarifa za tathimini ya athari ya mazingira;

v. Kuainisha aina ya miradi ambayo itahitaji ukaguzi wa athari kwa mazingira na ufuatiliaji;

vi. Kusimamia utekelezaji wa viwango vya usafi wa mazingira na kuhakikisha kuwa viwango hivyo vinafuatwa;

vii. Kuandaa mbinu na kuweka mikakati ya uzuiaji wa ajali ambazo zinaweza kusababisha uharibifu wa mazingira;

viii. Kushirikiana na Wizara na wadau wengine kuandaa mipango yenye lengo la kutoa elimu ya mazingira na kuongeza uelewa kwa umma juu ya umuhimu wa kuwepo kwa usimamizi bora wa mazingira;

ix. Kutoa na kusambaza machapisho na vitabu vya miongozo kuhusu usimamizi wa mazingira na uzuiaji au upunguzaji wa uharibifu wa mazingira; na

x. Pale inapowezekana, kutoa ushauri na msaada wa kiufundi kwa taasisi mbalimbali zinazojihusisha na usimamizi wa maliasili na mazingira ili kuziwezesha kutekeleza wajibu wao ipasavyo.

**Wadau wa Mazingira**

Kila mmoja aliyeko hapa kwa nafasi yake ni mdau wa shughuli za Mazingira. Usimamizi wa mazingira ni jukumu letu wote katika jamii, kwa kuzingatia ukweli huo, muundo wa kitaasisi umeainisha na kufafanua majukumu na uwajibikaji kwa ngazi zote za uongozi na utawala kuanzia ngazi ya kitongoji hadi ngazi ya Taifa. Sheria hii imetoa nguvu za kisheria za kusimamia mazingira kwa Mamlaka na Taasisi zifuatazo:-

1. ***Waziri Mwenye Dhamana ya Mazingira na mamlaka yake***
   Msimamizi Mkuu wa Masuala ya mazingira

2. ***Mkurugenzi wa Mazingira***
   Mratibu na Mshauri Mkuu wa Serikali (Waziri) kuhusu masuala yote ya Mazingira.

3. ***Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira***
   Kusimamia udhibiti, utekelezaji, uzingatiaji, upitiaji upya na upelembaji wa tathmini ya athari kwa mazingira na, kwa ajili hiyo, litawezesha ushirikishwaji wa umma masuala ya mazingira.

4. ***Wizara za Kisekta***

Kwa mujibu wa Kifungu cha 30 cha Sheria ya Mazingira Wizara za kisekta zina majukumu Kuhakikisha kuwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inafuatwa na kutekelezwa katika Wizara husika.

5. ***Sekretariati za Mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa***

Kwa mujibu wa Kifungu cha 34 cha Sheria ya Mazingira, Sekretariati za Mikoa zina jukumu la kuratibu shughuli za ushauri kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika mikoa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zina wajibu wa kusimamia Sheria ya Mazingira katika maeneo yao kuanzia Mkoani hadi katika ngazi za vitongoji.

**Ndugu Mgeni Rasmi**

**Lengo la kushirikisha mamlaka mbalimbali**

Lengo la kuwaita wadau mbalimbali kutoka katika mamlaka husika katika mkutano huu ni kutoa rai kwa wadau wote wa Mazingira kuhakikisha tunashiriki sote kwa pamoja kuhakikisha mazingira yetu yanatunzwa na yanaendelea kuwa salama.

**Lengo la kuwaita Waandishi wa Habari**

Kama sote tujuavyo, wanahabari wanatekeleza kazi muhimu ya kuielemisha na kuihabarisha jamii. Habari ama taarifa nyingi za mazingira huifikia jamii kupitia kazi za waandishi wa habari. Aidha taarifa muhimu za mazingira zenye ubora mkubwa pia hupatikana katika magazeti na majarida.

Baraza limeona ni vema sana kuwashirikisha wanahabari ili kupitia kwenu liweze kutoa maelekezo ya mambo muhimu kwa wadau kuhusu utunzaji wa Mazingira hususani kama ilivyojitokeza katika shughuli za ukaguzi wa utunzaji wa mazingira unaoendelea katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kwingineko nchini. Hivyo,

wanahabari MTUSAIDIE kuihabarisha jamii juu ya umuhimu wa utunzaji mazingira zikiwemo zile za kuchukua tahadhari.

**Ukaguzi wa shughuli za Mazingira katika Miradi mbalimbali**

Katika kukabiliana na changamoto za utunzaji/uchafuzi wa mazingira, Baraza (NEMC) liliunda vikosi kazi (Monitoring Task Force) kwa ajili ya kufuatilia kwa kina utekelezaji wa shughuli za mazingira katika miradi mbalimbali ya uzalishaji na maendeleo.

Lengo la ukaguzi wa shughuli za mazingira ni kubaini viwango vya uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira pamoja na kanuni mbalimbali katika uendeshaji wa miradi.

Ukaguzi wa kina umeshafanyika katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, baadhi ya miradi ya mkoa wa Dar es Salaam, Kanda ya Mashariki na Kanda ya Kaskazini. Na kwa wakati huu ukaguzi umefanyika Kanda ya Ziwa. Shughuli za ukaguzi wa mazingira katika miradi imekusudiwa kuwa zoezi endelevu na la kudumu ambalo litahusisha kanda zote, na kisha kurudia kwenye kanda ambazo tayari zimepitiwa ili kuhakiki utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa kwenye ukaguzi wa awali.

Kwa takribani miezi miwili na nusu (May-July 2016), Baraza (NEMC) limefanya ukaguzi wa mazingira katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mara na Kagera ili kufuatilia shughuli za utunzaji wa Mazingira katika miradi mbalimbali ya uzalishaji na maendeleo. Ukaguzi huu utaendelea pia kufanyika katika Kanda zote nchini.

**Matokeo ya ukaguzi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini**

Jumla ya miradi (facilities) iliyokaguliwa ni **200** ikiwemo:

1. Viwanda **Ishirini na tano (25)** vilikaguliwa ikijumuisha Usindikaji na uzalishaji;

2. Migodi **(95)** ikijumisha migodi mikubwa, ya kati na Mitambo ya uchenjuaji wa dhahabu;
3. Vituo vya **mafuta hamsini (54);**
4. **Hotel nane (8);**
5. Majengo ya biashara na makazi **kumi na nane (18);**

**Idadi ya miradi iliyokaguliwa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu Mara na Kagera.**

| Aina za Miradi | Migodi | Viwanda | Vituo vya Mafuta | Hoteli | Majengo |
|---|---|---|---|---|---|
| Idadi | 95 | 25 | 54 | 8 | 18 |

Jumla ya Miradi iliyokaguliwa ni **200**

Kutokana na ukaguzi uliofanyika miradi iliyokaguliwa imegawanywa katika makundi 3 kama ifuatavyo:

i. Miradi ambayo inatekeleza na kufuata matakwa ya sheria, kanuni na taratibu za utunzaji wa mazingira.

ii. Miradi ambayo imekuwa ikijitahidi kufuata sheria na taratibu za mazingira, lakini bado hawajafanya vya kutosha ili kufikia viwango vya mazingira vya ki-Taifa.

iii. Miradi isiyokuwa na mpango madhubuti wa hifadhi ya mazingira, hivyo kuvunja sheria, kanuni na taratibu za usimamizi na utunzaji wa mazingira.

**Jumla ya Miradi 200 ilikaguliwa**

| **No.** | **Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| 1 | Miradi inayotekeleza sheria ya mazingira kwa kiasi cha kuridhisha | 2 |
| 2 | Miradi ina vibali vya mazingira lakini haizingatia utekelezaji wa sheria na mpango wa kutunza mazingira mazingira (EMP) | 12 |
| 3 | Miradi inayotekelezwa bila vyeti vya mazingira | 86 |

**Mafanikio katika utunzaji mazingira**

Ukaguzi umebaini kuwa miradi michache imeonyesha utunzaji mzuri wa mazingira katika miradi yao. Baraza limeipongeza miradi iliyofanya vizuri na kuitaka kuzidisha juhudi katika utunzaji wa mazingira.

**Mapungufu yaliyoonekana katika miradi mbalimbali**

Upungufu mkubwa katika miradi iliyo mingi ulionekana katika maeneo mbalimbali ya miradi iliyokaguliwa kama ifuatavyo:

i. Baadhi ya miradi haina vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira,
ii. Utunzaji mbaya wa mazingira mahala pa kazi (poor housekeeping),
iii. Kutokuwa na mifumo mahususi ya utunzaji takangumu na majitaka,
iv. Utirilishaji wa maji taka yasiyosafishwa na kuingia katika vyanzo vya maji na mazingira,
v. Kutokuwa na miundo mbinu mahususi ya utunzaji bora wa mchanga wenye mabaki ya kemikali aina ya ***cyanide/mercury*** (ambayo ni sumu) kunakopelekea uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha afya za binadamu na mazingira kwa ujumla,
vi. Kutokuwa na miundo mbinu ya kutenganisha mafuta na maji (oil-water separator),
vii. Umwagaji hovyo wa vilainishi na mafuta, na utupaji ovyo wa machujio ya mafuta/vilainishi (oil filters),
viii. Kutozingatiwa kwa masharti na maelekezo yaliyoanishwa na kuambatanishwa katika vyeti na vibali vya mazingira,
ix. Utunzaji mbaya wa kemikali hatarishi kama vile ***cyanide***, tindikali n.k.

**Maelekezo yaliyotolewa na Baraza**

Kutokana na matokeo ya ukaguzi huu, Baraza limefanya yafuatayo:

i. Limetoa maelekezo ya kitaalamu kwa matatizo ya mazingira yaliyoonekana wakati wa ukaguzi,
ii. Limetoa adhabu ya faini, kusimamishwa na kufungiwa kwa baadhi ya miradi kutegemeana na kosa la ukiukwaji wa sheria na kiwango cha athari inayoweza kutokea katika mazingira kama miradi hiyo itaendelea kutekelezwa katika hali ya sasa, na
iii. Kuwataka wale wote ambao miradi yao haijafanyiwa TAM kuisajili mara moja miradi hiyo katika Baraza na kupata maelekezo zaidi,

## TAMKO LA BARAZA / MAMBO YA KUZINGATIWA

A. Baraza linawaagiza wale wote ambao hawajafanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira wafanye hivyo mara moja,

B. Miradi yote iliyokaguliwa na kupewa maelekezo na Baraza wanapaswa kuyatekeleza kwa wakati, kama walivyoelekezwa.

C. Kumekuwepo na ongezeko la miradi ya Uchenjuaji wa dhahabu. Ieleweke kwamba miradi hii inayotumia kemikali aina ya cyanide ni lazima ifanyiwe TAM ili kuweka miundo mbinu ya kuzuia athari zinazoweza kutokea,

D. Baraza linatoa onyo kwa wale wote ambao wamekuwa wakiwalaghai wawekezaji kwa madai kuwa ni washauri waelekezi wa mazingira. Baraza litaendelea kuwasaka na litachukua hatua kali dhidi yao,

E. Baraza linatoa wito kwa wawekezaji wote nchini kutoa kipaumbele katika utunzaji wa mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu,

F. Baraza linatoa wito kwa wawekezaji wote nchini kuhakikisha wanalipa ada na tozo za mazingira za kila mwaka ipasavyo na kwa wakati,

G. Sheria ya mazingira ya mwaka 2004 ni sheria mama inayohusiana na mambo yote ya mazingira hapa nchini. Hivyo Baraza linatoa wito kwa vyombo vya Serikali na wadau wote nchini kurejea sheria hii pale ambapo sheria zao zinapokinzana na Sheria hii.

H. Maafisa mazingira katika ngazi mbali mbali ni watendaji wakuu wanaosimamia mazingira na ni tegemeo la Serikali na wananchi kwa ujumla katika kuitekeleza Sheria.

## HITIMISHO

*Baraza linapenda wawekezaji wawekeze ili wapate faida kwa uwekezaji wao, watanzania wapate ajira na kuboresha maisha yao, serikali ipate kodi kuinua hali ya uchumi wa nchi yetu. Wakati wakizingatia sheria na leseni nyinginezo vilevile wazingatie sheria ya mazingira ambayo imelenga kulinda mazingira yetu na afya zetu kwa vizazi vyetu na vijavyo*

Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, ndugu wanahabari na wadau kutoka mamlaka mbalimbali tunatambua kuwa ninyi ni wadau wetu wakubwa katika kutunza mazingira. Kazi za utunzaji mazingira ni zetu sote wananchi. Hivyo, TUSAIDIANE kufikisha katika jamii taarifa za umuhimu wa utunzaji mazingira zikiwemo zile za kuchukua tahadhari.

Kazi hii ya ukaguzi wa shughuli za mazingira itakuwa endelevu, itafikia miradi yote nchini. Hapa napenda kutoa rai kwa wadau wote wa Mazingira nchini kuhakikisha tunashiriki sote kwa pamoja kuhakikisha mazingira yetu yanatunzwa na yanaendelea kuwa salama. NEMC itaendelea kufanya yafuatayo:

i. Kutoa elimu ya mazingira kwa wananchi na wadau mbalimbali wa mazingira kuhakikisha wanakuwa na ufahamu mzuri kuhususiana na Sheria ya Mazingira na Kanuni mbalimbali za mazingira,
ii. Kuwasisitizia wawekezaji kujali na kuzingatia sheria, kanuni, na taratibu zilizowekwa na serikali katika kuendesha miradi yao,
iii. Kuwakumbusha na kutoa adhabu kwa wale wote ambao wanavunja Sheria ya Mazingira na kanuni zake.

***<u>Asanteni sana kwa kunisikiliza na karibuni muulize maswali.</u>***

***<u>Kiambatisho;</u>*** **kutakuwa na Jedwali lenye kuonyesha miradi yote iliyokaguliwa, aina ya miradi, jumla ya fedha zilizotozwa (tozo za mazingira na adhabu/fine) na zilizolipwa.**